**HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA**

**TOVUTI:** www.ruvusecondary.sc.tz
**SIMU:**0713313310**( MKUU WA SHULE)**
0716626465**(MAKAMU MKUU WA SHULE)**
**0755970137/ 0713943193 (WALIMU MALEZI)**
**0716724562 (MWALIMU TAALUMA)**

SHULE YA SEKONDARI RUVU
**S.L.P 72**
**MLANDIZI**

TAREHE……………

**KUMB.NA RSS/MS/189/2022**
MWAFUNZI…………………………..
S.L.P………………………………………
…………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO 2022/23**

1.0 **UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ruvu kwa Mwaka wa masomo **2022/2023** Tahasusi (combination) ya …………………………….. Unapaswa kufika Shuleni tarehe…………………………kabla ya saa 11 jioni bila kukosa ukiwa umevaa sare ya Shule.

2.**0 JINSI YA KUFIKA SHULENI:**

Shule ipo Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani Km 77 kutoka Dar es salaam kando ya barabara kuu iendayo Morogoro. Ni kati ya Mlandizi na daraja la Mto Ruvu.

2.1 Kutoka Mbezi – DSM utafika Mlandizi na baadae tumia usafiri wa Bajaji au Taksi kuja shuleni. (Unashauriwa kutotumia usafiri wa pikipiki kwa tahadhari ya ajali kwani hii ni barabara kuu.)

2.2 Kutoka Mikoa mingine shuka kituo cha RUVU JKT KLABU na kisha vuka barabara kuja shuleni ambapo ni umbali mfupi tu kutoka uliposhukia.

3.0 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

| NA | MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | **Ada ya Shule** | **Sh. 70,000.00 kwa mwaka** |
| | | **Sh. 35,000 .00 kwa muhula** |
| 2. | **Taaluma** | **Sh. 20,000.00 kwa mwaka** |
| 3. | **Tahadhari** | **Sh. 5,000.00 haitarejeshwa** |
| 4. | **Ukarabati wa Samani** | **Sh. 15,000.00 mara moja** |
| 5. | **Matibabu( huduma ya kwanza)** | **Sh. 10,000 .00 kwa mwaka** |
| 6. | **Malipo ya vibarua(ulinzi na upishi)** | **Sh. 30,000.00 kwa mwaka** |
| 7. | **Kitambulisho** | **Sh. 5,500.00 mara moja** |
| 8. | **Kukodi godoro** | **Sh. 10,000.00 kwa mwaka** |
| 9. | **Mtihani wa kupijima(Mock)** | **Sh. 20,000.00 kwa mwaka** |
| 10. | **Nembo ya shule** | **Sh. 2500.00** |
| | **JUMLA** | **Sh. 188,000.00** |

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya Shule **NMB A/C Na. 21201200100** Jina la akaunti ni **RUVU GIRLS HIGH SCHOOL**. Malipo yote yajumuishwe kwenye fomu ya Benki (BPS) moja tu ambayo mwanafunzi atatakiwa kuiwasilisha shuleni siku anayoripoti ikionyesha Jina kamili la Mwanafunzi na tahasusi yake. Hakikisha unabaki na nakala moja ya karatasi ya Benki.

**NB: MALIPO YOTE YA SHULE YALIPWE BENKI. HATUPOKEI PESA TASLIMU ZA ADA NA MICHANGO YA SHULE ILIYOORODHESHWA HAPO JUU KATIKA JEDWALI**.
KUMBUKA KUANDIKA JINA KAMILI LA MWANAFUNZI

4.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**: Tafadhali mzazi tekeleza yafuatayo:

4.1 **SARE YA SHULE KWA KUZINGATIA RANGI NA MSHONO**

4.1.1 **Sare ya Darasani ni:**

- Sketi mbili ndefu za rangi ya kijani mkolezo(**Dark green**) zishonwe Marinda boksi . Ziwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu na si vinginevyo (Kitambaa kimeambatanishwa).
- Mashati meupe (Tomato) ya mikono mifupi mawili(2)
- Soksi ndefu (Free size) nyeupe jozi mbili au zaidi
- Sweta ya kijani mkolezo(Dark green) yenye shingo V
- Aje na tai ya kijani yenye michirizi myeupe iliyokatiza.
- Viatu vyeusi vya kufunika vyenye kisigino kifupi jozi mbili (visiwe na urembo)
- Tisheti ya pinki yenye nembo ya shule. Ni vema aje kununua maeneo ya jirani na shule ili kupata nembo ya shule.

  **NB:** Kwa wanaovaa hijabu watashona nusu kanzu nyeupe (badala ya shati) yenye urefu wa kufunika mikono na ifike chini ya makalio. Aidha ushungi (juba) uwe mweupe wenye kufunika mikono usio na urembo wowote.

4.1.2 **Sare ya Kushindia ni:**

- Mwanafunzi ashone gauni ya solo ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu kitambaa kimeambatanishwa. Kitambaa kiwe kizito (sio tetroni). Kuepuka kukosea rangi unashauriwa kuja kununua kitambaa hiki katika maduka yaliyopo jirani na shule.
- Viatu vya wazi (simple shoes)vyenye kisigino kifupi

  **NB:** Kwa wanaovaa hijabu ya kushindia iwe ya rangi ya bluu mkolezo(Dark blue) ya kitambaa kizito yenye kufunika mikono na isiwe na urembo.

4.1.3 **Sare ya Michezo ni:**

- Track suit ya rangi ya bluu bahari (Light blue) yenye mistari myeupe pembeni na isiwe ya kubana pamoja na fulana yake yenye rangi hiyo hiyo yaani jezi.
- Aje na raba nyeupe jozi moja

4.1.4 **Sare ya Maabara:**

- Mwanafunzi anayesoma masomo ya sayansi PCB, PCM, CBA na CBG ashone koti jeupe lenye urefu mpaka chini ya goti kwa ajili ya matumizi wakati wa practical. Aidha kwa anayesoma **Baolojia** awe pia na **Dissecting kit**

4.1.5 **Sare wakati wa kujisomea jioni (Evening Preparation)**

- Mwanafunzi ashone suruali ya kitambaa cha Bluu mkolezo (Dark bluu) kizito na iwe pana(Isiyobana)
- Mwanafunzi aje na fulana / tisheti nyeupe yenye kola maarufu kama form six isiwe na maandishi wala urembo wowote.
- Aje na soksi nyeusi ndefu(free size)

  **ZINGATIA** Sare za Shule zitavaliwa na mwanafunzi kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni kwa kuzingatia ratiba ya masomo, kazi za nje na michezo. Aidha mwanafunzi atavaa sare ya shule atokapo nje ya shule na anaposafiri kwenda likizo na kurudi shuleni. Ni marufuku kuja na mavazi mengine ya nyumbani au kuvaa urembo, kunyoa kipara, kusuka au kufuga nywele, kutumia madawa ya nywele na ya kujichubua, kupaka rangi kucha au midomo. Mwanafunzi hatakiwi kuvaa pete, bangili, hirizi au hereni.

  **NB;** Sare zote ziwekwe alama kwa kuandika jina la mwanafunzi ili kuepuka usumbufu wa kubadilishana au upotevu

## 4.2 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.

Mzazi /mlazi anatakiwa kuchangia huduma za elimu kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi awapo shuleni kama ifuatavyo:

4.2.1 Bunda (Ream) moja ya karatasi aina ya **A4** kwa muhula.

4.2.2 Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

4.2.3 Sanduku la bati (tranka) na kufuli imara, pia begi la madaftari. Masanduku mengine hayaruhusiwi.

4.2.4 Shuka nne za rangi nyeupe pamoja na mto na foronya nyeupe

4.2.5 Vibanio vya kuanikia nguo

4.2.6 Chandarua ya kuzuia mbu ya pembe nne rangi nyeupe(isiwe ya duara)

4.2.7 Ndoo ndogo ya kuogea pamoja na vyombo vya chakula (yaani kikombe, kijiko na kontena) kwa kuzingatia rangi zilizoelekezwa zifuatazo:

| Na. | TAHASUSI/COMBINATION | RANGI |
|---|---|---|
| 1. | PCB | Nyekundu (Red) |
| 2. | PCM | Bluu (Blue) |
| 3. | CBG | Njano (yellow) |
| 4. | CBA | Kijani (Green) |
| 5. | HGL | Pinki (Pinc) |
| 6. | HGK | Kahawia (Brown) |
| 7. | HKL | Blue bahari(Light blue |

**NB:** Mwanafunzi aweke alama kwa kuandika jina lake katika vifaa vyake vyote, pia asisahau kopo la Kuogea kulingana na rangi ya tahasusi/combination yake.

4.2.8 Tochi ya Betri au taa ya Sola kwa tahadhari umeme ukikatika

4.2.9 Madaftari makubwa (Counter Books) sita (6) au zaidi

4.2.10 Scientific Calculator kwa Wanafunzi wa Masomo ya Jiografia na Sayansi

4.2.11 Kitambulisho cha Bima ya afya (NHIF) kwa walionacho. Kwa asiye na Bima ya afya aje na **Sh. 55,000**(Elfu hamsini na tano)tu kwa ajili ya kukatiwa Bima hiyo

4.2.12 Nakala/kopi ya cheti cha kuzaliwa

4.2.13 Nakala/kopi ya hati ya matokeo ya kidato cha nne(statement of results).

4.2.14 Picha moja (1) ya passport size

4.2.15 Oxford advanced learners dictionary 1 na kamusi ya Kiswahili sanifu kwa masomo ya lugha

4.2.16 **VIFAA VYA USAFI**: Kila mwanafunzi alete vifaa vya usafi kama ilivyoainishwa hapo chini kulingana na Tahasusi:

1. **CBA:** Watering can, Brashi za kusugulia choo 2 na Gum boots 1 pair
2. **PCB:**Ufagio wa chelewa wenye mpini, jembe na soft broom
3. **PCM:** Ufagio wa chelewa wenye mpini,kwanja na rubber squeezer
4. **CBG**: Ufagio wa chelewa wenye mpini, kwanja na soft broom
5. **HGL**: Ufagio wa chelewa wenye mpini, soft broom na fagio la kutolea buibui
6. **HGK**: : Ufagio wa chelewa wenye mpini, Hard bloom na fagio la kutolea buibui
7. **HKL**: Ufagio wa chelewa wenye mpini, Rubber sqeezer na fagio la kutolea buibui.

**NB**: Kila mwanafunzi anapaswa kuleta vifaa vya usafi vilivyoainishwa na sio fedha taslimu. Vifaa vyote vitakaguliwa wakati mwanafunzi anaposajliwa.

## 5.0 **MENGINEYO**

5.1 Ni jukumu la mzazi/mlezi kumpatia mwanafunzi fedha kwa ajili ya matumizi binafsi awapo shuleni pamoja na kugharamia usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Fedha hizi apewe mwanafunzi mkononi, mzazi akadirie vema matumizi ya mwanae ili asiwe mbadhirifu au mdokozi.

5.2 Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha afya bora ya mwanae kwa kumpatia matibabu stahiki kabla ya kuja shuleni. Mwanafunzi mwenye maradhi ya kudumu aje na barua ya uthibitisho kutoka kwa daktari wa hospitali ya Wilaya, Mkoa au Rufaa. Aidha mwanafunzi apatiwe fedha za matibabu kwa dharura itakayojitokeza.

5.3 Mwanafunzi awe na vifaa vya usafi binafsi kama vile doti moja ya kitenge (asije na kanga),nguo za ndani,taulo za kike (Pads), taulo, mswaki, sabuni, mafuta ya kupakaa n.k(manukatoha yaruhusiwi)

5.4 Ni mategemeo yangu makubwa kwamba Mwanafunzi atasoma kwa bidii, atatoa ushirikiano kwa Wenzake, kwa Walimu na Watumishi wengine na atazitii kanuni na sheria za shule katika kipindi chote awapo shuleni ili kuleta ufanisi na maendeleo ya shule.

5.5 Kila mwanafunzi aandike jina lake katika sare zake zote za shule pamoja na vifaa vyake vyote binafsi ili kuepuka kuchangia ua kupotea

5.6 Kabla ya kuripoti shuleni mwanafunzi ajaze fomu zifuatazo na aje nazo:

- 5.6.1 Fomu ya taarifa ya Mwanafunzi na ya kukubali kujiunga na Shule.( Ijazwe na Mwanafunzi na kuthibitishwa na Mzazi)
- 5.6.2 Fomu ya uchunguzi wa afya( Medical examination form)

5.7 Mzazi/Mlezi: Mawasiliano yote yamhusuyo mwanao yafanyike kupitia namba za simu zilizo katika Fomu hii. Epuka mawasiliano na mtu mwingine asiejulikana ili usitapeliwe. Usitume pesa kwa Mtu yoyote atakayekupigia bila kupata uthibitisho toka Shuleni.

5.7 Hatupokei wanafunzi siku za Jumamosi, Jumapili, sikukuu na usiku(kwa sababu za kiusalama)

**MWANAFUNZI ASIJE NA SIMU YA MKONONI KWANI HAZIRUHUSIWI SHULENI NA WALA HAKUNA SEHEMU YA KUZIHIFADHI. AIDHA MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.**

**TAFADHALI SOMA KWA UMAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO ENDAPO KUNA KIPENGELE HUJAKIELEWA FANYA MAWASILIANO ILI KUPATA MAELEKEZO SAHIHI.**

Karibu sana Ruvu Sekondari
"Elimu ni Ukombozi"

**CHIMAZI,J C**
**MKUU WA SHULE**

## TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la mwanafunzi kama lilivyotumika katika mtihani wa kidato cha nne

   ………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi. Tarehe……Mwezi……….Mwaka………….
3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi

   i. Kijiji……………………

   ii. Wilaya………………….

   iii. Mkoa…………………..

4. Kabila la mwanafunzi…………………………………………………………..

5. Jinsia ya mwanafunzi……………………………………………………………

6. Dini yake/dhehebu………………………………………………………………………….

7. Jina la baba mzazi……………………………………………………………  PICHA

   Nambari yake ya simu………………………………………………………….

8. Jina la mama mzazi…………………………………………………………  PICHA
   Nambari yake ya simu…………………………………………………………..

9. Kama analelewa na mlezi, Jina kamili……………………………………………  PICHA

   Uhusiano na mwanafunzi…………………………………………………………

   Nambari yake ya simu……………………………………………………………

10. Shule ya Sekondari alikotoka mwanafunzi………………………………………..

11. Jina la mwenyekiti wa serikali ya mtaa……………………………………………..
    Nambari yake ya simu…………………………………………………………………

12. Je ana magonjwa sugu? Kama ndio taja……………………………………………..
    Anatibiwa hospitali gani…………………………………………………………….

Jina mzazi ……………………………..  Sahihi ……………………

Tarehe………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA.**
**SHULE YA SEKONDARI RUVU**

(**ANUANI YA MZAZI)**

…………………………

…………………………

YAH: **HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI RUVU.**

Mimi………………………………(Jina la Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi) wa …………….......

……………………(Jina la mwanafunzi)
Aliyekuwa akisoma Shule ya …………………………………..(Taja jina la Shule aliyosoma

mwanafunzi) katika Wilaya ya …………….Mkoa wa ……………. Ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari Ruvu iliyoko katika mji wa Mlandizi kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za Shule akikaa Shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili ya kidato cha tano na cha sita.
2. Kwamba kwa muda wote huo wa miaka miwili sitamsumbua Mkuu wa Shule, Afisa Elimu Sekondari Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

**Sahihi ya mzazi** **Tarehe**

…………………… …………………..

**AHADI YA MWANAFUNZI**.

Mimi…………………………………Nimekubali nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari Ruvu. Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA, KANUNI** na **TARATIBU** halali zilizopo, pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa Shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitazopangiwa.

**Jina la mwanafunzi** **Sahihi**

……………………………….. ……………………….

**Tarehe**……………………….

**SHULE YA SEKONDARY RUVU**
**FORM YA UCHUNGUZI WA AFYA**
**(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)**

This form is to be complete by Medical Officer

Name of Student:……………………………………Age……….Sex……………

The above named student has been examined in respect of:

I. STOOL…………………………………………………………………………

II. URINE………………………………………………………………………..

III. PREGINANCY……………………………………………………………..

IV. CHEST…………………………………………………………………………

V. BLOOD…………………………………………………………………………

VI. EYESIGHT…………………………………………………………………..

VII. HEARRING…………………………………………………………………..

VIII. HEART………………………………………………………………………..

IX. T.B……………………………………………………………………………..

X. STOMACH ULCERS……………………………………………………….

XI. COMMENTS

………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer………………………………..Designation…………………………

Station………………………..Signature and Stamp……………………..Date…………………

**HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA**
**SHULE YA SEKONDARI RUVU**

## 1.0 SHERIA ZA SHULE

Katika jamii yoyote ile ni lazima kuwepo SHERIA, KANUNI na TARATIBU zitakazowezesha jamii hiyo kuishi kwa kufuata maadili mema na mazuri, ili kufikia malengo yanayotarajiwa. Hivyo Ruvu Sekondari ina SHERIA, KANUNI na TARATIBU ambazo kila mwanafunzi lazima azifuate.

## 1.1 MAHUDHURIO

Wanafunzi wote wanatakiwa:

i. Kuwepo shuleni wakati wote na kufuata kwa makini ratiba ya kila siku kuanzia muda wa kuamka hadi muda wa kulala.
ii. Kuhudhuria na kuwahi vipindi vya darasani, vipindi vya elimu ya kujitegemea, michezo na shughuli nyingine zozote za shule kama zitakavyopangwa katika ratiba ya shule isipokuwa kama ruhusa ya kutokuwepo itatolewa.
iii. Kuleta vielelezo na / au taarifa ya kimaandishi kutoka kwa mzazi/ mlezi au/na daktari kueleza sababu za msingi za kutokuwepo shuleni.

**Mwanafunzi yeyote atakeyekiuka sheria hii kifungu 1.1 ( i) hadi (iii), atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**
**NB: Endapo mwanafunzi hatahudhuria shuleni kwa siku tisini mfululizo bila ya Kutoa taarifa yoyote atasimamishwa masomo au/ na atafukuzwa shule kabisa.**

## 1.2 TABIA NA MWENENDO

Mwanafunzi haruhusiwi kutenda yafuatayo:

i. Utoro.
ii. Uzururaji.
iii. Uasherati na uzinzi.
iv. Wizi na uongo.
v. Uvutaji bangi au ulevi wa aina yoyote ile.
vi. Utumiaji wa madawa ya kulevya.
vii. Kuchezea, kuharibu au kudharau alama za Taifa kama Bendera na Wimbo wa Taifa.
viii. Kupigana, kutukana au kuzomea.
ix. Kutoa lugha ya matusi kwa yeyote yule.
x. Kugomea masomo, adhabu na maagizo yoyote yaliyotolewa.
xi. Fujo na uchochezi.
xii. Kutofanya mtihani na mazoezi kwa makusudi na bila taarifa maalumu.
xiii. Kuficha maovu, wahalifu na uhalifu.
xiv. Makosa ya jinai.
xv. Kupata na kutoa mimba.
xvi. Kulala zaidi ya mwanafunzi mmoja kwenye kitanda kimoja.
xvii. Kufunika mapazia kuzunguka kitanda (kujenga “magheto” bwenini).
xviii. Kuolewa.
xix. Kutumia usafiri wa pikipiki ( bodaboda) anapokuja au kuondoka shuleni.
xx. Kutumia vibaya mali ya umma na hivyo kusababisha uharibifu na hasara.
xxi. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu.

i. Kuingia vilabuni, nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.

ii. Kumiliki simu ya mkononi vifaa vinavyoendana na simu na vifaa vinavyotumia umeme.
iii. Kumiliki vifaa vyenye ncha kali mfano visu, panga, bisibisi n.k.
iv. Kufanya biashara ya aina yoyote ndani ya shule.

**Mwanafunzi yeyote atakayetenda jambo lolote tajwa katika kifungu 1.2 (i) hadi (xxv) atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kumjulisha mazazi/mlezi, kusimamishwa masomo au/ na kufukuzwa shule kabisa.**

**1.3. HESHIMA**

Wanafunzi wote wanatakiwa:

i. Kutii kengele.
ii. Kuvaa sare ya shule kwa unadhifu na kwa kufuata ratiba ya uvaaji wa sare hiyo.
iii. Kusimama kwa unadhifu na ukakamavu wakati wa paredi.
iv. Kusimama na kusalimia wafanyakazi wote na wageni.
v. Wasitoke darasani bila ruhusa.
vi. Wasipige kelele madarasani na mabwenini.
vii. Waheshimiane wao kwa wao na wawaheshimu viongozi wao.
viii. Kuwaheshimu watu wote waliopo shuleni pamoja na maeneo ya jirani yanayozunguka shule na nje ya shule.

**Mwanafunzi atakayekiuka kifungu 1.3 (i) hadi (vii) atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

**1.4. MAVAZI**

Mwanafunzi anatakiwa avae sare ya shule kulingana na ratiba ya siku.
Mwanafunzi haruhusiwi:

i. Kuvaa kofia, viatu vya ghorofa ( high heels ) au/ na mapambo mengine yoyote.
ii. Kuwa na nywele ndefu.
iii. Kusuka nywele au kunyoa mitindo(style) ikiwemo kipara.
iv. Kufuga kucha ndefu za mikono na miguu au kupaka kucha rangi.

**Mwanafunzi yeyote atakayetenda jambo tajwa katika kifungu 1.4 (i) hadi (vi), atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**
**NB: Mwanafunzi atakayevaa mavazi yasiyo rasmi (Sare) yasioidhinishwa atanyang'anywa na hayatarejeshwa kwake**

**1.5. UTUNZAJI MALI**

Wanafunzi wote wanatakiwa

i. Kutunza mali na vyombo vya shule kama vile vitabu, madawati, meza, viti na majengo kwa ujumla. Ni marufuku kuandika chochote katika mali hizo.
ii. Kutunza mali zao wenyewe na zile walizokabidhiwa kwa matumizi yao wawapo shuleni.
iii. Kurejesha vifaa vyote vya shule kama vitabu na vingine kila wakati shule inapofungwa kwa mapumziko.
iv. Kutohamisha kifaa chochote kutoka mahali pake bila idhini. Endapo samani itahamishwa kwenye vyumba vya madarasa kwa ajili ya kujisomea/shughuli yoyote zirejeshwe kwenye vyumba husika bila kuchanganywa kuepuka usumbufu na uharibifu.

**Mwanafunzi yeyote atakayeshindwa kutimiza jambo lolote katika kifungu 1.5 (i) hadi (iv) atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.**

**NB: MWANAFUNZI ATAKAYESABABISHA UPOTEVU AU UHARIBIFU WA MALI YA SHULE ATALIPA MALI ALIYOPOTEZA/ALIYOHARIBU KWA GHARAMA HALISI YA MALI HIYO.**

## 2.0. CHAKULA

Chakula Cha wanafunzi kitapatikana shuleni. Hakutakuwa na chakula maalumu. Wanafunzi wote watakula chakula kilichoidhinishwa shuleni. Mwanafunzi haruhusiwi kubeba au kuagiza chakula kutoka nje ya shule.

**Atakeyekiuka kifungu 2.0 atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake**.

## 3.0. KUBADILI MAJINA AU ANUANI

i. Endapo jina la mwanafunzi au anuani ya mzazi/ mlezi vitabadilika kwa sababu yoyote ile, taarifa ya kimaandishi itolewe shuleni ili rekodi ziwekwe sahihi.
ii. Majina yaliyoandikishwa shuleni ndiyo yatakayotumika bila kubadilishwa.
iii. Jina la mwanafunzi linaweza kubadilishwa endapo hati maalumu ya mahakama itaambatanishwa kwenye maombi ya kubadili jina.

**Mwanafunzi atakayebadilisha anuani, jina, au kutumia majina yasiyo maalumu (nick names) kama yanavyosomeka kwenye usajili, atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

## 4.0 WAGENI

i. Wageni hawaruhusiwi kufika shuleni kuonana na mwanafunzi wakati wowote awapo shuleni. Iwapo kuna tatizo kubwa mfano kifo, taarifa zitolewe kwa Mkuu wa Shule. Utaratibu wa kumjulisha mwanafunzi utatolewa na Mkuu wa Shule.
ii. Pale itakapolazimu, wazazi/walezi watapokelewa shuleni siku za kazi kuanzia saa tatu (3:00)Asubuhu hadi saa nane mchana.
iii. Wageni wote wafike mapokezi kwanza kabla ya kumwona mwanafunzi.
iv. Mwanafunzi haruhusiwi kuzungumza/kuonana na mgeni bila ruhusa.
v. Wageni wataelekezwa eneo la kukaa. Ni marufuku kukaa na mgeni sehemu isiyo rasmi.
vi. Wazazi/walezi hawaruhusiwi kufika shuleni siku za Jumamosi, Jumapili na sikukuu.

**Mwanafunzi yeyote ambaye Mzazi/Mlezi wake atakiuka kifungu 4.0 (i) – (v) atakuwa ametenda kosa. Adhabu itatolewa dhidi ya mwanafunzi.**

## 5. MWISHO

Sheria, Kanuni na Taratbu hizi zisomwe mara kwa mara ili kuzielewa, kuzifuata na kuziishi wakati wote mwanafunzi awapo shuleni.



**VAZI LA DARASANI**



**VAZI LA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS)**



KOTI LA MAABARA KWA WANAFUNZI WA MASOMO YA SAYANSI



SWETA YA SHULE

**GENERAL STUDIES**

1. JOANNNES BIGIRWAMUNGU (etalal)5th Edition 2019 UNDERSTANDING GERERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL APE DSM.
2. NYAMBARI NYANGWINE UNDERSTANDING GENERAL STUDIES NOTED BOOK.
3. MBALASE BOOK 1 & 2
4. GENERAL STUDIES FOR V & VI BY MWAIPAJA M (2018)

**CHEMISTRY**

1. CONCEPTUAL CHEMISTTRY,DR.S.K.JAIN(S.CHAND) I & II
2. PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL-TIE (2019)
3. ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SEC. SCHOOL –TIE (2019)
4. INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SE.SCHOOL-TIE (2019)
5. GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SEC.SCHOOL –TIE (2019)
6. RAYMOND CHANG GENERAL CHEMISTRY.

**BIOLOGY**

1. BIOLOGY SCIENCE BY SOPER
2. TIE FORM 5 & 6 BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SEC.SCHOOL.
3. UNDERSTANDING BIOLOGY GLENN & SUZAN TOOTE.

**GEOGRAPHY**

1. HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY BY GOH CHONG LEONG, GILLIAN C.MORGAN
2. GEOGRAPHY ,AN INTERGRATED APROACH BY DAVID WAUGH.
3. PRACTICAL GEOGRAPHY BY PITCHERD.
4. ELEMENTARY PHYSICAL GEOGRAPHY BY AHMED LUBWAMA.
5. MAPSHEET KUBWA.

**PHYSICS**

1. PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE BY TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION (TIE)
2. PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL D SECONDARY SCHOOL FORM SIX BY TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION(TIE)
3. ADVANCED LEVEL PHYSICS (NELKON & PARKER)
4. ADVANCED LEVEL PHYSICS (KIRTH GIBBS)
5. PRINCIPLE PHYSICS REVIEWS (NECTA)
6. PRINCIPLE OF PHYSICS XI(S.CHAND'S)
7. PRINCIPLE OF PHYSICS XII(S.CHAND'S)
8. UNDERSTANDING PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL (JM BREITHAUPT)
9. UNIVERSITY PHYSICS(HUNG D YOUNG)
10. ADVANCED PHYSICS (TOM DUNCAN)

**BAM**

1. TIE–BASIC APPLIED MATHEMATICS.

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. PURE MATHEMATICS 1 & 2 BY BACKHOUSE
2. ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS BY C.J TRANTER.
3. SCIENTIFIC CALCULATOR FX-991.
4. CHAND'S
5. REVIEW $P_1$ & $P_2$
6. SYLLABUS
7. GRAPH PAPER
8. MATHEMATICAL SETS.

**ENGLISH**

1. A BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN BY AYI KWEYAMA
2. A MAN OF THE PEOPLE BY CHINUA ACHEBE
3. HIS EXALLENCE THE HEAD OF STATE BY DANSAFO
4. THE WONDERFUL SUGEON BY CHARLES MLOKA
5. BETRAYAL IN THE CITY BY FRANCIS IMBUGA
6. AN ENERMY OF THE PEOPLE BY ERICK IBSEN
7. A COMPLETE COURSE IN COMMUNICATION SKILLS BY KADEGHE
8. I WIL MARRY WHEN I WANT BY NGUGI WA THION'G & NGUGI WAMII
9. THE REAL ENGLISH TEXT BOOKS FOUR ADVANCED BY KADEGHE 2010.
10. SELLECTED POEMS BY TIE
11. THE OXFORD ADVANCED LEARNERS DICTIONARY
12. ADVANCED LEVEL ENGLISH A PRACTICAL APPROCH BY NICHOLOUS ACHERY.

**HISTORY**

1. ESSENTIAL ISSUE HISTORY PAPER 1 & II BY YASIN
2. MAJOR ISSUES IN HISTORY I & II BY YASIN.

**KISWAHILI**

1. KISWAHILI -1 (KIDATO CHA 5 & 6 ) BY KILANGI ENOCK LUCAS
2. KISWAHILI -2 (NADHARIA YA FASIHI)KIDATO CHA 5 & 6.BY KILANGI ENOCK.
3. KISWAHILI -2 (TAHAKIKI YA KISWHILI) KIDATO CHA 5 & 6 .BY KILANGI ENOC LUCAS.
4. THAKIKI YA KISWAHILI - BY NYAMBARI NYANGWINE.
5. CHUNGUTAMU MWANDISHI - T.A.MVUNGI
6. FUNGATE YA UHURU- MOHAMED SEIF KHATIB
7. KIMBUNGA- HAJI G.HAJI
8. MAPENZI BORA - SHAABAN ROBART
9. VUTA N'KUVUTE -SHAFI ADAM SHAFI
10. MFADHILI - HUSEIN TUWA
11. USIKU UTAKAPOKWISHA - MBUNDA MSOKILE
12. KUFIKIRIKA - SHAABAN ROBART
13. KIVULI KINAISHI - SAID MOHAMED
14. NGUZO MAMA- PENINA MUHANDO
15. MORAN - EMMANUEL MBOGO
16. KWENYE UKINGO WA THIM EBRAHIM HUSSEIN.

**AGRICULTURE**

1. SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM ONE (1). PUBLISHED BY KE LITERATURE BUREAU.
2. SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM TWO (2). PUBLISHED BY KE LITERATURE BUREAU.
3. SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM THREE (3). PUBLISHED BY KE LITERATURE BUREAU.
4. SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM FOUR (4). PUBLISHED BY KE LITERATURE BUREAU.
5. LONGHORN SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM ONE (1). WRITTEN JULIUS MAILU, PETER SIGEI AND DANIEL CHEMIYOT.
6. LONGHORN SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM TWO (2). WRITTEN JULIUS MAILU, PETER SIGEI AND DANIEL CHEMIYOT.
7. LONGHORN SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM THREE (3). WRITTEN JULIUS MAILU, PETER SIGEI AND DANIEL CHEMIYOT.
8. LONGHORN SECONDARY AGRICULTURE; STUDENT'S BOOKS; FORM FOUR (4). WRITTEN JULIUS MAILU, PETER SIGEI AND DANIEL CHEMIYOT.
9. CERTIFICATE AGRICULTURE; PUPIL'S BOOK; FORM ONE (1) WRITTEN BY AGGREY NYANJ AND JACOB O KONYANGO.
10. CERTIFICATE AGRICULTURE; PUPIL'S BOOK; FORM TWO (2) WRITTEN BY AGG NYANJOM AND JACOB O KONYANGO.
11. CERTIFICATE AGRICULTURE; PUPIL'S BOOK; FORM THREE (3) WRITTEN BY AGG NYANJOM AND JACOB O KONYANGO.
12. CERTIFICATE AGRICULTURE; PUPIL'S BOOK; FORM FOUR (4) WRITTEN BY AGG NYANJOM AND JACOB O KONYANGO.
13. FARM EQUIPMENT, MACHINERY, STRUCTURE AND BUILINDINGS WRITTEN BY **L ANYANZO (FOUR BOOK REQUIRED)**